# MAMBO YALIYOSABABISHA MAENDELEO YA UISLAMU

Mwandishi Ndugu Gerhard

Uislamu ulizaliwa katika mji wa Maka, uliopo katikati ya jangwa la nchi kubwa iitwayo Saudi Arabia. Wenyeji walio wengi wa nchi hiyo walikuwa wafugaji walioishi katika mahema na kuhama kila mara majani yalipopungua.  Watu wa mjini walikuwa wafanya biashara na wakulima wenye mashamba yao nje ya mji.

Hapo zamani Waarabu waliabudu mawe au miamba *(watham)*. Waliamini kwamba miungu fulani waliishi katika miamba hiyo. Baadaye waliongeza sanamu zilizochongwa, lakini ni tatu tu zinazojulikana kwa majina.  Kutokana na mapokeo ya awali ya Kiislamu, tunajua kwamba jumla ya vyote, miamba na sanamu, vilivyoabudiwa ilikuwa 27 tu.

Ingawa siku hizi tunafahamu 'mahali patakatifu' pamoja tu ambapo Waislamu wanapatembelea wakati wa kuhiji *(hajj)*, yaani ile *Ka'aba* kule Maka (ambayo pia huitwa *baithu'llah,* maana yake nyumba ya Allah), palikuwa na *"Ka'aba* nyingine fulani pamoja na mahali pengine kadhaa pa kuabudu hata kabla ya wakati wa Muhammad."

"Mola wa mji huu" (Maka, Sura 27:91) alikuwa sanamu iliyoletwa kutoka nchi ya Moabu iliyoitwa Hubal (katika lugha ya Kiarabu, herufi za sauti [vokali] hazikuandikwa). Sanamu hiyo iliwekwa ndani ya *Ka'ba* na kuitwa Allah kama miungu yao mingine. Jina hilo lilitumiwa kwa kumwita 'mungu' yeyote.  Tunajua kwamba babu yake Muhammad alitafuta msaada na ushauri kutoka kwa *Hubal*.1 Kitabu cha Agano la Kale cha Hesabu sura 25:1-3 hueleza jinsi watu wa Moabu walivyomwabudu *Baali,* au tukitumia neno la Kiyahudi linalomaanisha 'huyu', walimwita *HaBaal*.  Maana ya *Baal* ni Bwana sawasawa na maana ya jina la Mungu *Jahwe*. Tukiyatafakari hayo kwa makini hatuna budi tujiulize: *Hubal = HaBaal = Allah?*  Asili yake ni huko Moabu?  Je, Mungu anamwonaje huyo *Baal?* Sisi kama Wakristo tunapata majibu ya maswali hayo katika Biblia.

Lakini wakati ule kulikuwa na Wayahudi pia walioishi huko Arabia, hasa katika mji uitwao Medina. Tunafahamu makabila manne kwa jina.  Wao, kama Wayahudi wengine, walikuwa wamefukuzwa nchini kwao Israeli baada ya Hekalu kuangamizwa, mwaka 70 B.K. Walikuwa na dini yao, ingawa inaonekana kwamba hawakufahamu Agano la Kale vizuri. Hata Wakristo kadhaa pia walikuwa wanakaa katika maeneo hayo ya Kiarabu, hasa kusini (Yemeni) na kaskazini (Syria). Tunajua habari ya *'Waraqa ibn Nauful,* ambaye alikuwa mjomba wake mkewe wa Muhammad wa kwanza, *Khadija.*  Katika kitabu cha Al-Bukhari na.1,3, imeandikwa kwamba alijua lugha ya Kiyahudi (Kiebrania) na "aliandika kutoka katika Injili ya Kiebrania kiasi ambacho Allah alimtaka aandike".  Bila shaka Muhammad

alijifunza mengi kutoka kwake pamoja na wengine kuhusu Mungu Mmoja na Injili, pamoja na Adamu, Nuhu, Ibrahimu, Musa, Daudi, Yona na Yesu Kristo. Ingawa yamebadilishwa sana, yapo maelezo mengi katika Kurani kuhusu watu hawa na wengine wanaotajwa katika Biblia.

Muhammad alikua katika mazingira na mapokeo hayo. Alizaliwa mwaka 570 B.K. na wazazi wake wote walikufa kabla hajatimiza miaka sita. Alilelewa na babu yake, ambaye anajulikana kwamba alifanya ushirikina. Je, Muhammad hakurithi utambuzi wake wa kishirikina? Tunajua kwamba "rafiki zake waliogopa kwamba alikuwa ameonewa kijicho", na kwamba mama yake "alitumia uchawi ili aondoe nguvu yake". Hata alipokuwa mtu mzima, "aliogopa giza kiasi cha kutoweza kukaa chini katika chumba mpaka taa iwashwe kwanza". Zaidi ya hayo, "alichukia msalaba kiasi cha kuvunja kila kitu kilicholetwa ndani ya nyumba chenye alama hiyo ya msalaba juu yake". "Huyo Mtume wa Allah alipopata upuuzio wa kiroho, kulikuwa na sauti iliyosikika karibu na uso wake iliyofanana na uvumi wa nyuki", aliumwa na kichwa vibaya sana, "kila mara alizimia na kufanana na mtu aliyelewa". "Uso wake ulijaa povu, akanguruma kama mwana wa ngamia".2 Inajulikana sana kwamba Muhammad alikataa sanamu zote na miungu yote, na kushikamana tu na *'tawhid',* yaani umoja wa Allah usioweza kugawanywa kwa njia yoyote. Kila Mwislamu anamfuata Muhammad katika kuamini umoja huo kama jambo la msingi kabisa katika imani yake.

Lakini je, Allah ni nani? Waislamu pamoja na Kurani, huamini kwamba Jahwe (Mungu wa Wayahudi na Wakristo) na Allah ni mungu yule yule. Lakini tunapochunguza kwa makini zaidi tunagundua kwamba tabia na sifa za Allah hutofautiana kabisa kimsingi na sifa na tabia za Mungu wa Utatu wa Biblia.

**Neno la Mwisho:**

Uislamu umejengwa juu ya msingi wa mambo ambayo Muhammad aliyapokea (au alidai kwamba aliyapokea) kutoka kwa Allah kumpitia "malaika Gabrieli [Jibril]". Ujumbe wa Kurani unapingana kabisa na misingi iliyofunuliwa katika Biblia, na kutokana na hayo Uislamu umepata kuwa dini inayopinga Ukristo kuliko nyingine zote. Kwa kuwa Ukweli na Uwongo haviwezi kutokana na chanzo kimoja, hatuna budi tukatae dini hiyo, inayoweka msingi hata wa matendo yake (hasa wakati wa kuhiji *[hajj]*) katika asili yake ya kishirikina na kipagani.

Hata hivyo, tuwe waangalifu tusitumie maarifa hayo kama silaha ya kuwashambulia Waislamu! Badala yake, ujuzi huo utusaidie kutambua ujanja wa adui mwenyewe, Shetani, ambaye alibuni dini hiyo. Ingawa Uislamu ni silaha mikononi mwake, Waislamu wenyewe ni wanadamu ambao Kristo aliwafia, kwa sababu anawapenda pia! Tunataka kufahamu mengi yawezekanayo juu yao, pamoja na dini yao, inayowafunga minyororo. Waislamu wanahitaji kuwekwa

huru na utumwa wa giza na kuokolewa kwa neema itokayo kwa Yesu Kristo peke yake!

1. Kwa maelezo zaidi, soma kitabu cha Kiingereza "Premises and Principles of Muslim Evangelism", by Gerhard Nehls, kinachopatikana kutoka Hamasa ya Milele.

2. Mishkat, Kitabu cha 1, uk. 354 na 358; Al-Waqqidi kama alivyokaririwa na W. Muir katika "The Life of Muhammad" uk.200; Ibn Ishaq: Sirat Rasoolallah na Mizanulhaqq, vilivyoandikwa na C.G. Pfander, uk. 345-356

---

**MANENO MUHIMU YA KIARABU**

Hajj - kuhiji, kwenda Maka kwa wakati uliopangwa kila mwaka
Ka'ba - mraba, pahali patakatifu pale Maka
Tawhid- umoja wa Allah usioweza kugawanywa kwa njia yoyote
Taurat - Torati, vitabu vya Agano la Kale hasa vile 5 vya kwanza
Injil - Injili, Agano Jipya.